DAVID CONSTATINE,
S.L.P ………………..
TANGA.

5/11/2024.

MWENYEKITI,
BARAZA LA USULUHISHI LA NDOA KATA YA USAGARA,
S.L.P 2020,
WILAYA YA MISUNGWI,
MKOA WA MWANZA.

Ndugu,

**YAH: BARUA YA MWITIKIO WA KUHUDHURIA KIKAO BARAZA**

Rejea kichwa cha Habari hapo juu,

Awali ya yote nakushukuru kwa kupokea barua hii. Naitwa **DAVID CONSTATINE**, ni mume halali wa **HAPPINESS ASIMWE.** Ningependa kufikisha maelezo yangu kuhusu tuhuma alizozitoa mke wangu mbele ya Baraza lako kwamba nimemtelekeza na sitoi huduma za watoto wetu.

Kwanza kabisa, napenda kusema kuwa tuhuma hizo si za kweli. Katika kipindi chote cha miaka minne ya ndoa, nimekuwa nikijitahidi kwa kadri ya uwezo wangu kutoa huduma za msingi kwa watoto wetu wote, ikiwa ni pamoja na kulipa ada za shule, gharama za matibabu na huduma nyingine muhimu. Hata hivyo, baada ya muda mrefu kugundua kuwa mke wangu alikuwa akiwatesa watoto wangu (niliowapata kabla ya ndoa), nililazimika kutengana naye kwa ajili ya ustawi wa watoto na familia yetu kwa ujumla na nikamuachia mali zote nilizochuma na tulizochuma kwa pamoja.

Pia, ningependa kueleza kuwa baada ya kutengana, nilikuwa nafanya kazi nchini Sudan kwa kipindi cha muda mrefu, lakini baada ya kurudi nchini Tanzania, nilijikuta sina kazi tena. Mpaka muda huu sina kazi. Hali hii imenifanya nisiwe na uwezo wa kuingia kwenye majadiliano kwa haraka na kuhusika na masuala ya familia, ingawa nimekuwa nikihudumia watoto kwa kadri ya uwezo wangu. Tafadhali rejea nyaraka za uthibitisho wa malipo niliyomtumia mke wangu, malipo ya ada na cheti kinachothibitisha ukomo wangu wa ajira

Nilipokea wito wa tarehe 26/11/2024, ambao ulinitaka kufika katika Baraza lako tukufu. Hata hivyo, kwa sababu zilizo nje ya uwezo wangu nilishindwa kufika kwani nilikuwa nipo Tanga na pia sikuwa na uwezo wa kifedha wa kusafiri hadi Mwanza kwa haraka. Kwa hiyo, naomba kama Baraza litapendezwa liweze kupanga tarehe nyingine ya kusikiliza tuhuma hizi nikifika kwenye uwezo wa kusafiri au, kama inavyowezekana, nipate fursa ya kusikilizwa kwa njia ya simu ili haki itendeke kwa pande zote mbili.

Natumaini ombi langu litatazamwa kwa ufanisi, na kuwa na hakikisho kwamba nitapata fursa ya kujibu tuhuma kikamilifu na kuhakikisha kuwa haki inatendeka.

Nashukuru kwa kuzingatia ombi.

Kwa heshima,



David Constatine
+255766868696